WCB
Workers Compensation
Board of Manitoba

Kuripoti Jeraha

Ikiwa utaumia
ukiwa kazini,
tupo hapa
ili kukusaidia.

Ikiwa utaumia ukiwa kazini, tupo hapa ili kukusaidia.

Muhimu

- Unayo haki ya kuwasilisha dai la WCB kama utajeruhiwa ukiwa kazini. Si halali endapo msimamizi wako atakuomba kutowasilisha dai hilo.
- Kama utajipata matatani kwa kuripoti jeraha katika WCB, wafanyakazi wetu wa huduma za ukubalifu wapo hapa kukusaidia. Piga simu nambari **204-888-8081**, nambari ya bila malipo **1-844-888-8081** au tuma baruapepe katika Compliance@wcb.mb.ca.

wcb.mb.ca

Chapisho hili linatolewa kwa taarifa ya jumla pekee. *The Workers Compensation Act (Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi)* wa Manitoba na Kanuni, na sera za WCB ndiyo mamlaka ya mwisho kwa usimamizi wa bima na madai.

Kuripoti Jeraha

Hakuna anayetarajia kuumia kazini, lakini mara nyingi sana majeraha ya kazini hutokea. Yanapotokea, Workers Compensation Board (Bodi ya Fidia kwa Wafanyakazi, WCB) ipo hapa kusaidia.

Kwenye WCB tunaelewa majeraha ya kazini na madhara yake kwa wafanyakazi na familia zao. Kutokana na hayo, tunajitahidi kurahisisha mchakato wa kuwasilisha madai.

Unachohitaji kufanya...

1. **Mwambie msimamizi wako haraka iwezekanavyo.** Kama huwezi kutekeleza kazi zako za kawaida kazini, mwulize msimamizi wako ama kampuni lako linayo programu ya kurudi kazini ambayo unaweza kuhusika nayo wakati ukipata nafuu.

2. **Pata huduma ya utunzaji wa afya** aharaka iwezekanavyo na kuwa na hakika **kumwambia mtoaji huduma wako wa utunzaji wa afya kwamba ulijeruhiwa ukiwa kazini.** Anafaa pia kufahamishwa kuihusu programu ya mwajiri wako ya kurudi kazini.

3. **Ukikosa kuwa kazini wakati fulani kwa sababu ya jeraha lako, pigia simu WCB haraka iwezekanavyo.** Piga simu **204-954-4100**, au simu bila malipo **1-855-954-4321** (8:00 asubuhi – 7:00 jioni, Jumatatu – Ijumaa) na umpe maelezo ya jeraha Mwakilishi wa Taarifa ya Dai.

Unapopiga simu, tafadhali kuwa na taarifa ifuatayo:

- nambari yako ya bima (social insurance number),
- nambari yako ya siri yenye dijiti tisa (personal health identification number),
- jina la mtoaji huduma ya afya uliyemtembelea kutokana na jeraha
- lako na taarifa yako ya ujira, kama vile hati yako ya malipo.

Baada ya kutoa maelezo ya jeraha lako, utapewa nambari ya madai na jina na nambari ya simu ya mwamuzi atakayeshughulikia dai lako. Mwamuzi ni mfanyakazi wa WCB atakayeshirikiana nawe kuhusu dai lako na mtu utakayewasiliana naye ukiwa na maswali yoyote.

Ikiwa utahitajika kulipia matibabu au gharama zozote zinazohusiana na jeraha lako, hifadhi stakabadhi zako halisi na umfahamishe mwamuzi wako. Gharama hizi zinaweza kushughulikiwa na WCB.

Kile msimamizi wako anachohitaji kufanya...

Msimamizi wako ana jukumu la kuripoti majeraha kazini kwenye WCB ndani ya siku tano za kufanya kazi baada ya kutambua jeraha. Lazima msimamizi wako pia akulipe kwa zamu nzima uliyokuwa unapaswa kufanya kazi siku uliyojeruhiwa, si tu kufikia wakati ulipojeruhiwa.

Msimamizi wako ana machaguo mbalimbali ya kuripoti majeraha ya kazini kwenye WCB.

1. Wanaweza kuripoti kielektroniki kwa kutumia *Online Incident Reporting System* (Mfumo wa Kuripoti Tukio wa Mtandaoni) kulingana na Intaneti ya WCB.

2. Wanaweza kuripoti kwa simu kwa kupiga simu *Claim Information Centre* (Kituo cha Taarifa cha Madai) cha WCB kwa nambari **204-954-4100** au simu bila malipo **1-855-954-4321**.

3. Wanaweza kujaza fomu ya *Employer's Incident Report form* (Ripoti ya Tukio la Mwajiri) ya WCB na kuituma kwa faksi kwenye WCB kwa nambari **204-954-4999** au simu bila malipo **1-877-872-3804**, au kutuma baruapepe ya ripoti iliyokamilika.

wcb.mb.ca

Kile mtoaji wako wa huduma ya afya anachohitaji...

Unapomtembelea mtoaji huduma ya afya kutokana na jeraha au ugonjwa wa kazini, mtoaji huduma ya afya:

- atajaza WCB Healthcare Report *(Ripoti ya Huduma ya Afya ya WCB)*, na
- kuituma kwa faksi kwenye WCB nambari **204-954-4999**, au simu bila malipo **1-877-872-3804**.

Ripoti za mtoaji wa huduma ya afya zinaweza kutumwa kwa njia ya barua WCB kwenye 333 Broadway, Winnipeg, MB R3C 4W3.

Kile WCB itakachokifanya...

Pindi tu WCB inapopokea taarifa kuhusu jeraha lako kazini, dai litafunguliwa na kupewa mwamuzi.

Kisha WCB:

- Itahakikisha kuwa jeraha lililotokea kwa sababu ya kuajiriwa kwako na kuthibitisha ukubwa wa jeraha lako kupitia mtoaji wako wa huduma ya afya
- kuamua faida unayostahili
- kuwasiliana nawe kukuambia uamuzi ni upi kwenye dai lako na unapotarajia kupokea faida na huduma.

Unachostahili kufanya unapopata **nafuu** kutokana na jeraha lako kazini...

1. **Fuata mpango wa mtoaji tiba yako wa huduma ya afya na uhudhurie miadi yote.**

2. **Wasiliana na msimamizi wako kila mara kuhakikisha kuwa anafahamu unavyoendelea na siku unayoweza kurejea kwenye kazi mbadala/ iliyobadilishwa au majukumu yako ya kazi ya kawaida.**

3. **Wasiliana na mwamuzi wako kila mara kuhakikisha kuwa mabadiliko yoyote muhimu kulingana na jeraha, nafuu, na uwezo wako wa kurejea kwenye kazi yako ya kawaida yamefahamika.**

Taarifa ya jumla usiyoweza kujua kuhusu WCB

- Mahali pako pa kazi hulipia faida zote za bima ya WCB – haziondolewi kwenye malipo yako wala kufadhiliwa na dola za ushuru.
- WCB inaendeshwa na Halmashauri ya Wakurugenzi inayojumuisha Mwenyeketi wa Bodi asiyeegemea upande wowote, wakilishi watatu wa wafanyakazi, wakilishi watatu wa wajiri na wakilishi watatu wa maslahi ya umma.
- WCB inajitolea kutoa huduma ya haraka, rahisi, ya kujali, ya haki na wazi.

WCB
Workers Compensation Board of Manitoba

Mshirika wa kuaminika, kukata bima leo na kuijenga kesho salama zaidi:

Ikiwa utaumia ukiwa kazini, tupo hapa ili kukusaidia.

Namna ya Kutufikia

Workers Compensation Board of Manitoba
333 Broadway, Winnipeg, MB R3C 4W3

Tutumie barua pepe
wcb@wcb.mb.ca

Kwa taarifa zaidi, tembelea
www.wcb.mb.ca

au tupigie simu
204-954-4321

au simu bila malipo
1-855-954-4321

Ripoti udanganyifu au uzembe

Piga simu 204-888-8081
au piga simu bure 1-844-888-8081
Barua pepe **Compliance@wcb.mb.ca**

Kazi SALAMA ni jukumu la kila mmoja. Kuzuia majeraha ni vizuri kwa waajiri na wafanyakazi. Kwa maelezo zaidi, tembelea kwenye:

safemanitoba.com

au piga simu 204-957-SAFE (7233)
ndani ya Winnipeg
au 1-855-957-SAFE (7233) nje ya Winnipeg

SAFE WORK MANITOBA

WCB1000SW-03/06/15 Swahili

CEP SCEP UNION LABEL